



## **JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

### **WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**

#### **TANGAZO LA VIJANA KUJIUNGA NA VITUO VYA JENGA KESHO ILIYO BORA (BBT) VYA UFUGAJI MIFUGO KIBIASHARA**

1. Wizara ya Mifugo na Uvuvi inakaribisha maombi ya Vijana kujiunga na vituo vya BBT vya ufugaji mifugo kibiashara ambapo watakaa kwa kipindi kisichozidi Mwaka mmoja katika maeneo yafuatayo:-
  - i. Uyui - Tabora
  - ii. Makuyuni - Arusha
  - iii. Mkata - Morogoro
  - iv. Ruvu - Pwani
  - v. Nangaramo - Mtwara
  
2. Waombaji watakuwa katika makundi matatu kama ifuatavyo:-
  - i. Asilimia 40 ya vijana watakaodahiliwa watatoka katika Halmashauri za Mkoa husika ambapo Mradi utatekelezwa na maombi yatatumwa kwa Katibu Tawala wa Mkoa husika (Anuani ya kila Katibu Tawala wa Mkoa husika imenakilishwa mwisho wa Tangazo hili),
  - ii. Asilimia 30 ya vijana watatoka katika Jeshi la Kujenga Taifa na majina yao yatawasilishwa na Mkuu wa JKT kwa Katibu Tawala wa Mkoa husika, na
  - iii. Asilimia 30 ya wadahiwa ni Vijana waliohitimu Mafunzo katika vyuo vya Mifugo kwa ngazi ya shahada, stahada au cheti. Maombi katika kundi hili yaelekezwe kwa Katibu Tawala wa Mkoa husika.
  
3. Sifa za waombaji
  - i. Awe Raia wa Tanzania,
  - ii. Awe na umri kati ya Miaka 18 – 30,
  - iii. Mwombaji awe ni Kijana mwenye tabia njema na Barua yake ya maombi iidhinishwe na uongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa anapoishi,
  - iv. Awe tayari kushiriki mafunzo kwa vitendo katika shughuli za ufugaji mifugo kibiashara katika kipindi husika,
  - v. Awe tayari kufuata miongozo na taratibu zilizowekwa katika kituo atakachokuwa akifanyia shughuli za ufugaji kibiashara, na
  - vi. Awe mwenye Afya njema itakayomwezesha kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa Mradi.

4. Fomu ya kujiunga na vituo hivi inapatikana kupitia tovuti za Wizara ya Mifugo na Uvuvi ([www.mifugouvuvi.go.tz](http://www.mifugouvuvi.go.tz)) na za Sekretarieti za Mikoa husika. Fomu ya Maombi kwa kundi namba 2(iii) iambatishwe nakala ya vyeti vya masomo vilivyothibitishwa. Aidha, waombaji wote wawasilishe nakala za vitambulisho vya NIDA vya mwombaji na nakala ya kitambulisho cha Mdhamini.
5. Fomu ya maombi na viambatisho vitumwe kupitia barua pepe za Mikoa husika.
6. Waombaji wataochaguliwa katika hatua ya kwanza wataitwa kwa ajili ya usaili kwa vitendo katika vituo walivyochaguliwa. Waombaji wawe tayari kujigharamia nauli, chakula na malazi wakati wa usaili kwa vitendo vituoni.
7. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 24/05/2024.
8. Maombi yawasilishwe kupitia barua pepe za Katibu Tawala wa Mikoa husika kama ifuatavyo:-

Mkoa wa Tabora: [ras.tabora@tamisemi.go.tz](mailto:ras.tabora@tamisemi.go.tz)

Mkoa wa Arusha: [ras@arusha.go.tz](mailto:ras@arusha.go.tz)

Mkoa wa Morogoro: [ras.morogoro@tamisemi.go.tz](mailto:ras.morogoro@tamisemi.go.tz)

Mkoa wa Pwani: [ras@pwani.go.tz](mailto:ras@pwani.go.tz)

Mkoa wa Mtwara: [ras@mtwara.go.tz](mailto:ras@mtwara.go.tz)

Kwa ufafanuzi zaidi, Wasiliana na:-

- i. Mkoa wa Tabora: Asanterabi Sangenoi – 0754 – 450183 AU Mussa H. Mussa - 0682058815
- ii. Mkoa wa Arusha: Dkt. Sabas P. Shange - 0756442966 AU Bw. Richard Nkini - 0754082195/0684057000
- iii. Mkoa wa Morogoro: Dkt.Gasper Msimbe – 0652434368/0620279198 AU Bw. Waziri Mahimbo - 0714752134
- iv. Mkoa wa Pwani: Elisante S.Qadwe – 0787302606 AU Dr. Ramadhani A. Mwaiganju - 0612600390
- v. Mkoa wa Mtwara: Dr. Subira Simbeye - 0785648115 AU Bw. Nanjiva Geoffrey - 0655353051